# Muundo na matumizi ya umiliki siachanifu kwa Kiswahili sanifu

***Odile Racine-Isa***
Taasisi ya Kitaifa ya Lugha na Tamaduni za Mashariki, Paris

**Ikisiri**
Katika Kiswahili sanifu inawezekana kuzungumza kuhusu kiumbe hai, mwili wake na hisia zake kwa njia mbalimbali. Njia iliyotumiwa kuliko zote ni umiliki siachanifu[1] kwa sababu mwili na sehemu zake ni kitu kimoja. Pia, upande wa kiisimu, umiliki siachanifu una mambo yake ya pekee ya kisarufi miundo. Makala hii, kwanza inazingatia sababu za kutumiwa kwa umiliki siachanifu; pili inazingatia mabadiliko yaletwayo na umiliki siachanifu kwenye valensi[2] ya vitenzi. Makala haichambui kabisa masuala ya kirai nomino. Inauliza tu kwa nini msemaji Mswahili hupendelea namna hii ya kusema wakati ambapo angeweza kutumia kanuni za kawaida za sarufi-miundo kuzungumzia mambo hayo hayo.

## 1.0 Umiliki siachanifu hutumiwa kuzungumzia nini?

Ukichukua riwaya mbili[3] na kuorodhesha matumizi yote ya umiliki siachanifu, utatambua kwamba unatumiwa kuzungumzia sehemu mbalimbali za mwili (moyo, mishipa, mdomo, miguu, mikono, macho, paji, malaika, nywele, nk.); majimaji mbalimbali ya mwili (damu, jasho, machozi, usaha, mate, mkojo, udenda, kamasi, nk.); ishara za uhai (sauti, mawazo, pumzi, nk.); hisia za kimwili (kutetemeka, kuhisi baridi, joto, maumivu, raha, njaa, kiu, usingizi, harufu, nk.); hisia za kimawazo (hofu, wasiwasi, wivu, kuhamaki, ujeuri, aibu, haya, nk.); sehemu za kiumbe zisizochukuka (roho, pepo, kivuli, picha, nk.);
pamoja na vitu vinavyoweza kugusa mwili (kiboko, sigara, moshi, kalamu, nk.); na meza na miguu yake, gari na magurudumu yake, nk. Hapa tunaweza kudhani kwamba ni kwa sababu kuna uhusiano baina ukamili wa kitu na sehemu zake mbalimbali.

## 2.0 Mambo ya pekee ya sarufi muundo ya umiliki siachanifu

Umiliki siachanifu huleta mabadiliko kwenye kanuni za kawaida za hali elekezi ya vitenzi. Kwa Kiswahili sanifu, ukitaka kubadilisha idadi ya vingoeshe[4] vya kitenzi fulani, inabidi ukite kiambishi cha unyambulishaji baina ya mzizi wa kitenzi na irabu tamati. Lakini, ukitumia miundo ya umiliki siachanifu, haina haja : kitenzi sielekezi hufuatwa na yambwa bila ya kuongezewa mofimu yoyote. Kwa hivyo, tutakachozingatia kwanza ni kanuni za kawaida za hali elekezi ya vitenzi. Baadaye tutachambua mambo ya pekee ya umiliki siachanifu.

### 2.1. Kanuni za kawaida za hali elekezi ya vitenzi kwa Kiswahili sanifu

Kwa Kiswahili hali elekezi ya vitenzi hutegemea 1) *valensi* ya kitenzi asili, 2) unyambulishaji. Kuna aina mbalimbali za unyambulishaji, nyingine huongezesha idadi ya vingoeshe vya kitenzi, nyingine hubakisha kingoeshe kimoja tu (kiima), nyingine hubadilisha dhima ya vingoeshe.

#### 2.1.1. Vitenzi bila ya unyambulishaji

[1] Ninamshukuru Profesa K. Kahigi kunisaidia kutafsiri kwa Kiswahili baadhi ya msamiati wa kiisimu nilioutumia kwenye makala haya.
[2] Mwanaisimu Mfaransa L. Tesnière (1959), alitumia neno la kisayansi *valence* kumaanisha idadi ya nomino kitenzi kimoja kinakubali pamoja na uhusiano wake na kitenzi hicho. Kamusi Sanifu ya Biolojia, Fizikia na Kemia (1990) imetafsiri *valensi* na kueleza kwamba ni "uwezo wa atomu kuungana". Tazama pia R. Ohly (1987), S. D. Irira (1995).
[3] *Vuta n'kuvute* cha Shafi Adam Shafi pamoja na kurasa 12 za *Utangano* cha Said A. Mohamed. Kwa jumla kurasa 300 na matumizi 149.
[4] Yaani nomino zote zinazo uhusiano na kitenzi kimoja.

Kwa kawaida, kwa Kiswahili, ikiwa kitenzi chenye vingoeshe viwili kimetumiwa, maneno hupangiliwa kama ifuatayo : kiima + kitenzi + yambwa. Kwa kawaida kwenye mpangilio huo, kiima kimechukua nafasi ya mtenda na yambwa imechukua nafasi ya kitendwa. Yambwa, ambayo hufuata kitenzi moja kwa moja (mfano wa [1]) hudokezwa na dokezo la yambwa[5] yaani kiambishi-ndani kinachotangulia mzizi wa kitenzi (mfano wa [2]). Kiambishi hicho hupatanishwa na nomino kinayoidokeza.

[1] Mwizi amevunja **mlango**. [6]

[2] Mwizi ame**u**vunja.

Kwenye mfano wa [2], dokezo la yambwa *–u-* (ngeli ya 3) linadokeza nomino *mlango* (ngeli ya 3) ya mfano wa [1] na kutosha kuiwakilisha.

### 2.1.2. Kauli ya kutendwa

Kauli ya kutendwa huashiriwa na *-w-* inayopachikwa baina ya mzizi wa kitenzi na irabu tamati. Mpangilio wa maneno ni : kiima + kitenzi + kijalizo, yaani : kitendwa + tendo + mtenda ambaye huingizwa na kiingizi *na*. Kwenye kauli ya kutendwa haiwezekani kupachika dokezo la yambwa kati ya kitenzi. Kwa mfano :

[3] Mlango umevunj**wa** **na** mwizi.

### 2.1.3. Kauli ya kutendea

Kauli ya kutendea, ambayo huashiriwa na *-i-* au *-e-* baina ya mzizi wa kitenzi na irabu tamati, hupanua *valensi* ya kitenzi yaani huongeza idadi ya vingoeshe. Kingoeshe kipya, ambacho huwa ni mtendewa, hudokezwa kwenye kitenzi na *dokezo la yambwa*. Mifano ya [4], [5] na [6] inaonyesha kwamba kauli ya kutendea inawezesha kitenzi asili chenye vingoeshe viwili (*mtu kuandika kitu)* kuwa kitenzi chenye vingoeshe vitatu (*mtu kum*w*andikia kitu mtu*).

[4] Mwalimu ameandika barua.

[5] Mwalimu ame**ni**andik**i**a barua.

Kwenye mfano huo wa [5], *dokezo la yambwa* (-*ni*-) linamdokeza mtendewa ambaye hakutajwa pengine.

[6] Mwalimu ame**mw**andik**i**a barua **mwanafunzi.**

Kwenye mfano wa [6], mpangilio wa maneno ni : kiima + kitenzi + yambwa 1 + yambwa 2, yaani : mtenda + tendo + mtendewa (ambalo limedokezwa kwenye kitenzi na kufuata kitendwa) + kitendwa (ambacho kimeambatana na kitenzi moja kwa moja). Kupachika dokezo hilo la yambwa kati ya kitenzi kunamsogeza mtendewa mpaka mwisho wa kauli.

[5] Kutokana na kwamba tutazungumzia mambo ya sarufi-miundo hatutatumia msamiati wa sarufi-maumbo. Kufuatana na shauri za D. Creissels (1991) na kwa nia ya kusisitiza uhusiano baina ya kiambishi (kwenye kitenzi) na nomino kinayoidokeza tutatumia maneno ya *dokezo la kiima* na *dokezo la yambwa* .

[6] Herufi nene zimetumiwa kusisitiza mambo tunayoyachambua.

### 2.1.4. Kauli ya kutendesha

Kauli ya kutendesha hupatikana kwa kukita unyambulishaji *–ish-, -iz-, -esh-* au *–ez-*[7]. Kauli hiyo ina utungo kama ule wa kauli ya kutendea yaani muundo wake wa kisintaksia ni kama ifuatayo : kiima + kitenzi + yambwa 1 + yambwa 2. Upande wa kisemantiki, maneno hayo yamechukua nafasi za : mtenda + tendo + mtendewa + kitendwa. Tofauti baina ya kauli ya kutendea na kauli ya kutendesha ni kwamba kwenye kauli ya kutendesha, mtendewa hushirikiana na tendo. Tulinganishe mifano ya [7] na [8].

[7] Mtoto anakula ndizi.

[8] **Mama** ana**mlish**a ndizi **mtoto**.

Kwenye mfano wa [8] kingoeshe kipya *mama* kimechukua dhima ya kiima, yaani mtenda. Mtenda/kiima wa sentensi asili (*mtoto*) amesogezwa kwenye hali ya mtendewa (Tazama Vitale, 1981 : 152-168) na kudokezwa kwenye kitenzi na dokezo la yambwa ya ngeli ya 1, nafsi ya 3 *–m-*. Kwa hivyo, kauli hizo za kutendea na kutendesha zinapanua *valensi* ya kitenzi. Ikiwa kitenzi asili ni kitenzi elekezi (yaani hufuatwa na yambwa/kitendwa) yambwa ya pili ni mtendewa. Kwa kawaida mtendewa ni binadamu, kwa hivyo yeye ndiye anayedokezwa na dokezo la yambwa kwenye kitenzi.

### 2.1.5. Kauli ya kutendeka

Kauli ya kutendeka, ambayo huashiriwa na *-k-* iliyokitwa baina ya mzizi wa kitenzi na irabu tamati, hupunguza *valensi* ya kitenzi elekezi cha asili, yaani kitenzi elekezi kikinyambulishwa kwa unyambulishaji wa kutendeka huwa kitenzi sielekezi. Matokeo yake, maneno yanayobakia ni : kiima + kitenzi, yaani : kitendwa + tendo. Haiwezekani kukita dokezo la yambwa kati ya kitenzi. Kwa mfano :

[9] Mlango umevunji**k**a.

### 2.2. Mabadiliko yanayoambatana na matumizi ya umiliki siachanifu

Matumizi ya umiliki siachanifu huambatana na mabadiliko ya kanuni za *valensi* ya kitenzi. Tumesema kwamba umiliki siachanifu hutumiwa kuzungumzia mtu anavyohisi kimwili au kimawazo. Lakini mtu anaweza kuhisi tuseme maumivu, kwa sababu ametafunwa na mdudu au kwa sababu amejitoga mwenyewe. Kwa hivyo sisi, tutatofautisha ikiwa kiumbe amemfanyia kitu kiumbe mwenzake au kama kiumbe amepatwa mwenyewe na hisia fulani.

Upande wa kisarufi, tukirudia kwenye mfano wa hali wa kwanza hapo juu, tunakuta kitenzi elekezi ambacho hufuatwa na yambwa moja tu, lakini kikitumiwa kwenye tengo la umiliki siachanifu kitenzi hicho hicho kitafuatwa na yambwa mbili. Tena, kama ilivyo kwa kauli za kutendea na kutendesha, *dokezo la yambwa* litamdokeza mtendewa. Kutokana na kwamba tungo hilo limeshachambuliwa kwa makini na wanaisimu (HARRIES, 1970 ; HINNEBUSH & KIRSNER,1980 ; SCOTTON, 1981) tutaichungulia kwa kifupi tu. Sisi tutasisitiza juu hali ya mfano wa pili hapo juu, yaani ikiwa tendo linamhusu kiumbe mwenyewe. Katika hali hiyo vitenzi sielekezi hufuatwa na yambwa, na dokezo la yambwa lililomo kati ya kitenzi humdokeza mtendewa vile vile.

### 2.2.1. Hali ya kwanza : mtenda na mtendewa ni viumbe viwili

Ikiwa mtu anamfanyia kitu mwenzake, dokezo la yambwa kwenye kitenzi humdokeza mtendewa. Ikiwa huyo mtendewa anatajwa, mara nyingi anasogezwa kwenye hatua ya pili baada ya kitenzi, yaani baada ya nomino inayomaanisha sehemu ya mwili. Kwa hivyo tungo la sentensi ni kama

[7] Kufuatana na kanuni za utangamano wa irabu wa unyambulishaji pamoja na irabu wa silabi tamati ya mzizi wa kitenzi. Kwa maelezo kuhusu kanuni hizo tazama kwa mfano E. Ashton, 1944 : 217, 230.

ifuatayo : kiima + kitenzi + yambwa 1 + yambwa 2. Tungo hilo linaambatana na : mtenda + tendo + kiumbe timamu (yaani *dokezo la yambwa* kwenye kitenzi) + sehemu ya mwili (yaani yambwa inayofuatana na kitenzi moja kwa moja). Kwa hivyo tukilinganisha muundo huo na tungo la kauli ya kutendea au kauli ya kutendesha tunaona kwamba hapa pia dokezo la yambwa linamdokeza mtendewa. Kwa mfano *:*

[10] Ali**m**kamata mkono **bi Tamima**. (S. A. MOHAMED, 1980)

Kwenye mfano wa [10] dokezo la yambwa *–m-* linalotangulia mzizi wa kitenzi *–kamata* limo kwenye ngeli ya 1. Ngeli hiyo hujumlishwa umoja wa nomino za viumbe hai. Kwa hivyo dokezo hilo linamdokeza bi Tamima (nomino ya binafsi) haliashirii *mkono* ambao ni nomino ya ngeli ya 3. Neno hilo *mkono* limechukua dhamira ya yambwa/ kitendwa.

Hata hivyo, kiumbe timamu hakitajwi kila mara. Pengine hukumbushwa na dokezo la yambwa kama mfano wa [11] unavyoonyesha.

[11] Aki**m**poza moyo na kumbembeleza ... (S.A. Mohamed, 1980)

Kwenye mfano huo, mizizi wa kitenzi *–poza* umetanguliwa na dokezo la yambwa la ngeli ya 1. Dokezo hilo linamkumbusha mtu ambaye ameshatajwa. Pamoja na hayo, kitenzi hicho kimefuatwa na yambwa kwenye ngeli ya 3 : *moyo*. Neno hilo linalomaanisha sehemu ya mwili, limechukua nafasi ya kitendwa.

Kwa hivyo, kwenye mifano hiyo miwili tunaona kwamba hakuna upatanisho baina ya dokezo la yambwa kwenye kitenzi (dokezo hilo huwa la ngeli ya 1 na hudokeza kiumbe timamu) na nomino iliyomo kwenye dhima ya yambwa kwa kuambatana na kitenzi moja kwa moja (na kudokeza sehemu ya mwili inayoathiriwa na tendo). Zaidi ya hivyo, vitenzi *–kamata* (mfano wa [10]) na –*poza* (mfano [11]) ambavyo, kwa kawaida, hufuatwa na yambwa moja tu, vimeambatana hapa na yambwa mbili bila ya kupachikiwa kiambishi cha unyambulishaji.

### 2.2.2. Hali ya pili : sehemu ya mwili kuchukua dhamira ya kiima/ mtenda

Mara nyingi umiliki siachanifu hutumiwa ikiwa mtu anahisi kitu mwenyewe. Katika hali hiyo, sehemu ya mwili huchukua dhamira ya kiima. Hapa ni kana kwamba sehemu ya mwili ingemfanyia kitu kiumbe kamili. Mpangilio wa maneno ni kama ifuatavyo : kiima + kitenzi + yambwa, yaani kiima ni mtenda na yambwa ni kitendwa. Pamoja na hayo kitenzi, ambacho kwa kawaida hukubali yambwa moja tu, hapa kinafuatwa na yambwa mbili bila ya kuongezewa kiambishi chochote cha unyambulishaji.

#### a) Vitenzi asili sielekezi

[12] Maneno yali**m**kwama, yakawa hayatoki kinywani mwake ... (S.A. Shafi, 1999:67)

Kwenye mfano wa [12], mzizi wa kitenzi *–kwama*, ambacho kwa kawaida ni kitenzi sielekezi, hapa kimetanguliwa na dokezo la yambwa -*m*- ya ngeli ya 1 (nafsi ya 3) linalomaanisha kiumbe kamili. Vile vile kwenye mfano wa [13], kitenzi *–jaa* ambacho kwa kawaida ni kitenzi sielekezi, hapa kimepachikwa dokezo la yambwa linalomdokeza kiumbe kamili.

[13] Yasmin aliinamisha uso chini hofu ime**m**jaa. (Shafi:1999:18)

#### b) Vitenzi kwenye kauli ya kutendeka

Kama tulivyoona hapo juu, vitenzi kwenye kauli ya kutendeka ni vitenzi sielekezi. Hata hivyo, ikiwa mtu anazungumzia hisia zake yaani akitumia tungo la umiliki siachanifu,, dokezo la yambwa hukitwa katikati ya kitenzi.

[14] Sasa **Yasmin** alianza kulia kwa sauti na machozi yana**m**tiririka. (S.A. SHAFI, 1999 : 98)

Kwenye mfano wa [14] mzizi wa kitenzi *–tiririka* umetanguliwa na dokezo la yambwa la ngeli ya 1 linalommaanisha Yasmin aliyetajwa mwanzoni mwa sentensi.

Kwa hivyo, kauli ya umiliki siachanifu, inakifanya kitenzi chenye yambwa moja kuelekeza yambwa mbili (mifano ya [10] na [11] ambapo mtenda ni mtu mwingine) na kitenzi sielekezi huelekeza yambwa moja (mifano ya [12], [13], [14] ambapo sehemu ya mwili imechukua nafasi ya mtenda). Kwenye mifano yote, dokezo la yambwa hudokeza kiumbe timamu ambaye aidha ni mtendewa, au kitendwa. Kutokana na mambo hayo, inabidi sasa tujiulize kama nafasi hizo za mtenda na kitendwa au mtendewa zinaendelea kujazwa namna hiyo tukibadilisha lengo la mawasiliano.

**2.3. Mabadiliko ya lengo mawasiliano.**

Katika uchambuzi ufuatao hatutazingatia ikiwa mtu anamfanyia kitu mwenzake bali ikiwa mtu anahisi kitu mwenyewe. Ina maana kwamba tutayaangalia mageuzi kutoka tungo sielekezi kuwa tungo elekezi. Hata hivyo hatutaangalia mabadiliko ya kitenzi kikingoesha vingoeshe viwili au vitatu.

Mabadiliko ya shabaha ya mawasiliano hupatikana aidha kwa kubadilisha mpangilio wa kawaida wa maneno aidha kwa kutumia kauli ya kutendwa. Kwa kila namna, kitendwa kitatangulia kitenzi. Kwa hivyo, kwenye tungo la umiliki siachanifu ndiye kiumbe kizima anayetarajiwa kutolewa mwangaza na kutangulia kitenzi.

**2.3.1 Mabadiliko ya mpangilio wa maneno**

**a) 2.1.1. Yambwa + kitenzi + kiima**

[15] **Yasmin** kili**m**toka kicheko. (s.a. Shafi, 1999:127)

Kwenye mfano wa [15], kiima *kicheko* (ngeli ya 7) kimedokezwa kwenye kitenzi na dokezo la kiima *ki-* (ngeli ya 7) lakini kimefuata kitenzi wakati yambwa (*Yasmin*) ipo mwanzoni mwa sentensi na kudokezwa kwenye kitenzi na *dokezo la yambwa* la ngeli ya 1 *-m-*.

**b) Yambwa + kiima + kitenzi**

[16] **Tamima** machozi yali**m**dondoka. (S. A. MOHAMED, 1980)

Kwenye mfano wa [16], yambwa (*Tamima*) ipo mwanzoni mwa sentensi lakini imefuatwa moja kwa moja na kiima (*machozi*).

**c) Kiima + yambwa + kitenzi**

Pia inawezekana kuweka yambwa kwenye hatua ya pili baada ya mwanzo wa sentensi, yaani baina ya kiima na kitenzi. Tazama jina la binafsi la *Biti Kocho* kwenye mfano wa [17].

[17] Mshipa wa ujuba Biti Kocho umeshamsimama. (S.A. Mohamed, 1980)

**2.3.2. Matumizi ya kauli ya kutendwa**

Ikiwa umiliki siachanifu unavifanya vitenzi sielekezi kuwa vitenzi elekezi, tunatarajia kukuta mifano ya umiliki siachanifu kwenye kauli ya kutendwa. Kutokana na mabadiliko yanayoletwa kwa kawaida na kauli hiyo, kitendwa kitachukua dhima ya kiima na mtenda ataingizwa na kiingizi *na*.

Hata kama sentensi hizi ni adimu zinapatikana. Ukimwambia msemaji Mswahili bila ya kumwelezea mazingira ya matumizi yake, mara nyingi atasema kwamba unajizonga na kukushauri matumizi ya kauli ya kutenda. Lakini ukimsomea aya ulipoikuta atakubali kabisa. Jambo la pekee la sentensi hizo ni kwamba hukutwa hadithi inapofika kileleni, yaani wakati simulizi inapopinduka na mambo yanapokuwa magumu sana kwa mhusika wa hadithi. Kwa mfano :

*A. Ufafanuzi wa mlipuko wa bomu :*

[18] **Watu** wengi walikuwa **wakichururikwa na damu** kutoka katika majeraha waliyoyapata kutokana na kujikata kwao kwa vioo. (S. A. SHAFI, 1999 : 137)

Kwenye mfano wa [18], kitenzi *–chururika*, ambacho huwa si kitenzi elekezi, hapa kimo kwenye kauli ya kutendwa na kufuatwa na kiingizi pamoja na mtenda - *damu*. Nomino *watu*, ambayo imechukua dhima ya kiima, inamaanisha wale walioathiriwa na tendo, yaani ni kitendwa.

*B. Barua ya mapenzi ambamo mwandishi anafichua hisia yake :*

[19] Kama ujuavyo binaadamu wameumbwa na haya, lakini wakati mambo yanapomzidi mtu **hutokwa na haya** …(S.A. Shafi, 1999:168)

*C. Mapigano ya kimwili mwili baina ya wasichana wawili waliosikilizana sana :*

[20] Vita vile viliendelea kila mmoja **akivujwa na matusi**, ... (S.A. Shafi, 1999:171)

Mwishowe baadhi ya vitenzi havipatikani kwenye kauli ya kutendwa isipokuwa ndani ya tungo la umiliki siachanifu tu. Kwa mfano :

[21]... alirejea nyumbani kwa haraka akiwa **amejawa** na furaha, ... (S.A.Shafi, 1999:35)

Kwa kawaida kitenzi -*jaa* ni kitenzi sielekezi kwa hivyo hakiwezi kutumiwa kwenye kauli ya kutendwa, lakini pamoja na umiliki siachanifu inawezekana. Vile vile kwa kitenzi -*ruka* kwenye mfano ufuataao :

[22] Alikuwa **karukwa** na roho. (S.A. Mohamed, 1980)

Kwa hivyo, kwa upande wa sarufi miundo, umiliki siachanifu unapanua valensi ya kitenzi. Lakini upanuzi huo unategemea masharti mbalimbali : 1) mada ya mazungumzo ni mwili na hisia yake ; 2) lazima kitendwa kiwe ni kiumbe kizima ; 3) ikiwa tendo linahusu undani wa mtu mwenyewe, sehemu ya mwili huchukua dhima wa kiima/ mtenda.

Mgawanyiko huo baina sehemu ya mwili/ mtenda upande mmoja, na ukamili wa mtu/ kitendwa upande mwingine, unaendelea kwenye kauli ya kutendwa hata kama vingoeshe hivyo vimebadilishana dhima yake ya kisarufi miundo.

## 3.0 Uchaguzi wa Umiliki siachanifu

Hata kama si kitu cha kawaida, inawezekana pia kuzungumza kuhusu mwili na hisia yake kwa kutumia utungo wa kawaida wa kisarufi miundo. Hivyo ndivyo ilivyo kwenye mfano wa [23].

[23] ... na kujiburura taratibu akiwa ame**u**kumbatia **moyo wake** ... (S.A. Shafi, 1999:106)

Kwenye mfano huu, mtu mwenyewe (aliyedokezwa na dokezo la kiima la nafsi ya 3 *a*-) amechukua nafasi ya mtenda wakati sehemu ya mwili (iliyodokezwa na dokezo la yambwa la ngeli ya 3 -*u*- yaani *moyo*) imechukua nafasi ya yambwa/ kitendwa. Ina maana kwamba msemaji

Mswahili anaweza kuchagua kutumia umiliki siachanifu au la. Kwa hivyo kwa nini anachagua matumizi hayo?

Tukizingatia njia mbalimbali za kusema *kukojoa* tunaona kwamba umiliki siachanifu unawezesha kusema kwamba tendo si la makusudi. Kwenye mfano wa [24] tunaona utungo wa kawaida : dokezo la kiima (*a*-) linalomaanisha kiumbe timamu/ mtenda + tendo (yaani mzizi wa kitenzi). Hapa tunafahamu kwamba tendo ni la makusudi.

[24] Amekojoa

Mfano wa [25] unaonyesha matumizi ya umiliki siachanifu kwenye kauli ya kutenda. Tunafahamu kwamba tendo halikutakiwa lakini, hata hivyo, matokeo si makubwa sana.

[25] Mkojo umemtoka.

Lakini kwenye mfano wa [26] si vigumu kuwaza masikitiko ya mtu akitambua matokeo ya tendo.

[26] Ametokwa na mkojo.

Kauli hii ni ya umiliki siachanifu kwenye kauli ya kutendwa. Tukizingatia maana yake, haitoshi kusema kwamba tendo halikuzuiwa, tunafahamu pia kwamba ni jambo kubwa limetokea.

**Hitimisho**

Tunaweza kusema kwamba matumizi ya umiliki siachanifu yanategemea chaguo la msemaji. Bila shaka chaguo hilo linagusia mambo ya kiutamaduni kwa sababu ni kama kusema kwamba hisia fulani ni kitu kisichotakiwa na mtu mwenyewe. Kinacholeta maana hiyo ni kwamba kila mara, ikiwa kwenye kauli yoyote, mtenda ni sehemu ya mwili na kitendwa au mtendewa ni kiumbe timamuzaidi ya yote, matumizi ya umiliki siachanifu kwenye kauli ya kutendwa yanasisitiza ushinde wa kuzuia tendo. Ni kama mtu angefanyika watu wawili. Labda hiyo ndiyo sababu vitenzi sielekezi vinonekane kana kwamba ni vitenzi elekezi. Lakini swali hilo la mwisho haliwezi kuhakikishwa au kukanushwa bila ya uchambuzi wa ujumla wa valensi ya vitenzi kwa Kiswahili sanifu kufanyika.

**Marejeo**


Ashton, E.O. (1944), tena: 1984) *Swahili Grammar. Including intonation*, Singapore, Longman

Creissels Denis (1991) *Description des Langues négro-afriaines et Théorie syntaxique*, Grenoble, Ellug.

Feuillet, Jack (1987) "L'organisation des trois points de vue*", Bulletin de la Société de Linguistique de Paris*, tome LXXXII, fasc. 1 : 1-41.

Harries Lyndon (1970) "Inalienable Possession in Swahili" *African Languages Review*, suppl. 9 : 140-147.

Hinnebusch Thomas J.& Kirsner Robert S. (1980) "On the Inference of Inalienable Possession in Swahili", *Journal of African Languages and Linguistics*, n°2/1 : 1-16.

Irira S.D. (1995) *Kamusi Awali ya Sayansi na Teknolojia*, Dar es-Salaam, Ben & Company Limited.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B., Msanjila, Y.P. (2001) *Sarufi ya Maumbo ya Kiswahili Sanifu*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) Dar es Salaam, Chuo Kikuu.

Kirkeby Willy A. (2000) *English Swahili Dictionary*, Dar es Salaam, Kakepela Publishing Company (T) LTD.

Lazard Gilbert (1994) *L'actance*, Paris, PUF.

Massamba, D.P.B., Kihore, M., Hokororo J.I**.** (1999, tena: 2001) *Sarufi ya Miundo ya Kiswahili Sanifu. Sekondari na Vyuo, Dar es-Salaam*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) na Chuo Kikuu cha Dar es-Salaam.

Mdee, James Salehe (1996) *Sarufi ya Kiswahili, Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam, DUP LTD.

Ohly, Rajmund (1987) *Primary Technical Dictionary. English-Swahili*, Dar es-Salaam.

Mohamed, Said Ahmed (1980) *Utengano*, Nairobi, Longman.

Scotton Carol Myers (1981) "Extending Inalienable Possession : The Argument for an Extensive Case in Swahili", *Journal of African Languages and Linguistics*, Leiden, vol. 3/2 : 159-174.

Shafi, Adam Shafi (1999) *Vuta n'kuvute*, Dar es-Salaam, Mkuki na Nyota Publishers.
Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2001) (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, Dar es-Salaam TUKI, UNESCO, SIDA..
Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2001) (1990) Kamusi Sanifu ya Biolojia, Fizikia na Kemia, Dar es-Salaam, TUKI, UNESCO, SIDA.
Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2001) *Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza*, *Swahili-English Dictionary*, Dar es Salaam, Chuo Kikuu.
Tasniere Lucien (1959, tena: 1988) *Éléments de Syntaxe Structurale*, Paris, Klincksieck.
Avitale, Anthony (1981) *Swahili Syntax*, Dordrecht – Holland/ Cinnaminson – USA.